

Jumapili 6 Januari, 2019

ZANZIBAR LEO

MICHEZO



MKURUGENZI wa jumuiya ya GOZA yenye makao makuu yake nchini Ujerumani Antje Fleischer, akimkabidhi vifaa vya michezo mchezaji wa Akademi ya Vijana ya Ujamaa Said Ali Salum, vilivyotolewa na jumuiya hiyo kusaidia harakati za michezo hafla iliyofanyika klabu ya Ujamaa Rahaleo. (PICHA NA AMEIR KHALID).

Ausems azungumzia ushindi

NA MWAJUMA JUMA
KOCHA wa Simba Patrick Aussems amesema walistahiki kupata ushindi kwenye mchezo wao dhidi ya Chipukizi, kutokana na kiwango walichokionesha wachezaji wake.

Kocha huyo aliyaeleza hayo mara baada ya kumalizika mchezo huo wa kombe la mapinduzi uliochezwa usiku wa kuamkia jana kwenye uwanja wa Amaan, ambapo ilishinda mabao 4-1.

Alisema kuwa wachezaji wake walicheza kwa kuonesha kiwango kikubwa cha soka ambacho kimemvutia sana.

Hata hivyo alisema kuwa kutokana na kiwango hicho walipaswa kufunga mabao zaidi ya waliyoyapata.

Aidha koča huyo alisema kuwa mashindano hayo ya kombe la mapinduzi yataweza kumsaidia sana katika maandalizi ya michuano vake